# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

**DKT. SAADA M. SALUM (MBM)**
**AKIWASILISHA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI MWAKA 2024 NA MPANGO WA MAENDELEO WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**KWA MWAKA 2024/2025**

**JUNI, 2024**

YALIYOMO:....................................................................................i
UTANGULIZI ..................................................................................1
MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023 NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2023/2024 ....................4
MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023..........................4
Mwenendo wa Uchumi wa Dunia ..................................................4
Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Duniani ........................................5
Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar ..............................................6
Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar .......................................7
Uingiaji wa Watalii ...........................................................................9
Mwenendo wa Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (Intra trade) ..................................................................................11
Ukuzaji Rasilimali ..........................................................................11
UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 .................................................12
Utekelezaji wa Maeneo ya Kimkakati kwa Kipindi cha Miezi Tisa (Julai 2023 – Machi 2024)..........................................................12
MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024 NA MPANGO WA MAENDELEO WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2024/2025 ................22
Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia ....................................................22
Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar ................................................22
MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/2025 .25
Maeneo ya Kimkakati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025...................25
RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/2025 ............................................29
MAENEO MTAMBUKA.......................................................................29
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI...33
MAJUMUISHO ................................................................................36
HITIMISHO......................................................................................38

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Ni heshima ya kipekee kutoa hoja kwamba Baraza lako lipokee na kujadili **Mpango wa Maendeleo Kwa mwaka 2024/2025.** Naomba kuwasilisha Hotuba ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2024/2025 inayoambatana na **Kitabu cha Kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi 2023 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 na Kitabu cha Pili cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi 2024 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2024/2025.** Taarifa za vitabu hivyo zimezingatia **Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050; Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025;** Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa wakati wa **Ufunguzi wa Baraza la Kumi (10) la Wawakilishi** na ahadi anazozitoa anapokutana na wananchi; **Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya Mwaka 2015-2030; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC) ya mwaka 2050; pamoja na Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya Mwaka 2050.**

2. **Mheshimiwa Spika,** ninamshukuru Mungu kwa kutujaalia neema ya uhai na afya njema iliyoniwezesha kuwasilisha kwa mara nyengine **Hotuba ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2024/2025.** Mwaka mmoja ni kipindi kikubwa kwa maisha ya binadamu, wako ambao wamepatwa na ugonjwa na wako ambao wametangulia mbele ya haki katika kipindi hiki. Namuomba Mwenyezi Mungu awasamehe wazee na ndugu zetu waliotangulia mbele ya haki na sisi tuliobakia atuzidishie afya njema, hekima na busara katika mijadala ya kikao hiki na vyengine. Ninamshukuru Mungu kwa kulijaalia Taifa letu amani, utulivu na mshikamano na kwa kutuwezesha kukutana katika Mkutano huu wa Baraza la Kumi (10) la Wawakilishi ili kujadili namna ya kuharakisha maendeleo

ya Taifa kupitia Bajeti zilizowasilishwa katika Baraza hili la kujadili Bajeti.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa, ninapenda kumshukuru **Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** ambaye ameendelea kuniamini kwa kunipa dhamana ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango. Miongozo yake na uongozi wake mahiri, vinatusaidia sisi wasaidizi wake tuweze kufikia maono na malengo ya nchi. Kipekee, na kwa muktadha wa majukumu ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha **Diplomasia ya Uchumi** iliyochochea kuongezeka kwa mashirikiano baina ya nchi yetu na nchi rafiki, kuvutia wawekezaji binafsi na kuimarisha mazingira ya uwekezaji pamoja na kuitangaza nchi yetu kuwa kivutio na mahala salama kutembelea na kuwekeza. Sisi sote ni mashahidi wa ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa ahadi zake alizozitoa kwa wananchi. Utaratibu aliouanzisha Rais wetu wa ufuatiliaji wa shughuli za Serikali zikiwemo shughuli za maendeleo ambazo zinamuwezesha kufahamu kwa karibu utekelezaji wa maagizo na ahadi zake. Miongoni mwa shughuli alizozisimamia kwa nguvu zake zote ni pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya usafirishaji, huduma za afya, elimu, maji, umeme pamoja na mawasiliano. Tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kuilinda na kuitunza miundombinu hiyo na rasilimali nyengine za nchi kwa manufaa ya wananchi wote na vizazi vijavyo. Mafanikio haya ni juhudi na uono wake wa kuleta mapinduzi ya kiuchumi na kijamii katika kuinua hali za wananchi Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia nitoe pongezi za dhati kwa **Makamo wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** wakiwa wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais kwa uongozi wao mahiri, usimamizi, uchapakazi na uzalendo kwa nchi yetu. Juhudi zao zinasaidia kukuza na kuimarisha ustawi wa nchi yetu na wananchi kwa ujumla. Nichukue fursa hii pia kumpongeza

**Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said** kwa kusimamia **Utumishi wa Umma** na kutoa miongozo kupitia Kamati ya Makatibu Wakuu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu wote kwa ujumla awape umri na afya njema waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

5. **Mheshimiwa Spika,** ninamshukuru kipekee na kwa dhati kabisa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.** Muungano wetu ni tunu yetu na tunafurahia mashirikiano yaliopo baina ya viongozi wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni ishara ya kukomaa kisiasa na kidemokrasia. Uongozi wake wa busara unasaidia uimarishaji wa uchumi na huduma za kijamii. Kwake tunafurahia muelekeo mpya na usiotetereka wa kuimarisha uwajibikaji katika sekta ya umma, kupambana na vitendo vya rushwa na ubadhirifu na kuimarisha ulinzi wa mali za Taifa.

6. **Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa **nikushukuru wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid** kwa kusimamia na kuendesha vyema vikao vya Baraza letu kwa ufanisi mkubwa. Hii inaonesha wazi ujasiri na busara unazotumia katika kutekeleza majukumu yako ikiwemo kuendesha shughuli za Baraza. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima, afya na uweledi katika utendaji wa kazi zako za kila siku. Shukrani nyengine pia ziende kwa viongozi wetu wa Baraza wakiwemo **Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti; kwa umahiri wao katika kuendesha Baraza.** Aidha pia, niipongeze na kuishukuru sana Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kwa umakini wa miongozo waliyotupatia muda wote wa mzunguko wa kazi zetu.

7. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi na shukrani, sasa naomba kuwasilisha kwa muhtasari Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2023, Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 pamoja na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2024/2025.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023 NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2023/2024

**8.** **Mheshimiwa Spika,** Mapitio haya ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2023 yamezingatia viashiria vya Uchumi Mkuu (Macroeconomic Indicators) ikiwemo Pato la Taifa, Kasi ya Mfumuko wa Bei, Ajira, sekta ya nje; na Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 ambao umezingatia hali ya utekelezaji halisi na kifedha kwa programu na miradi ya maendeleo.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023

### *Mwenendo wa Uchumi wa Dunia*

**9.** **Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi Duniani (World Economic Outlook) ya mwezi Aprili 2024 inaonesha kuwa kwa mwaka 2023, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imefikia wastani wa asilimia 3.2 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kumetokana na kupungua kwa uzalishaji kwa baadhi ya nchi zilizoendelea, mabadiliko ya sera za kifedha kwa nchi zilizoendelea ili kupunguza athari za kupanda kwa bei na kuongezeka kwa gharama za mikopo.

Taswira ya ukuaji wa uchumi wa dunia imegawanywa katika makundi kama ifuatavyo: -

i. **Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Zilizoendelea (Developed Economies)** ambao umefikia wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.7 kwa mwaka 2022. Ukuaji huo umetokana na mabadiliko ya sera za kifedha ambayo yameanza kuleta athari kwa nchi hizo;

ii. **Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibuka Kiuchumi (Developing and Emerging Economies)** umefikia wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2022. Hali hii imesababishwa na ongezeko la malighafi kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji na uzalishaji viwandani pamoja na ujenzi wa miundombinu;

iii. **Kwa Nchi za Afrika,** kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022. Kutokana na kupungua kwa usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara, uuzaji wa mafuta ghafi pamoja na kupungua kwa uzalishaji wa madini kwa baadhi ya nchi za Afrika;

iv. **Kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (Sub Saharan Countries),** kasi ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2023 imefikia wastani wa asilimia 3.4 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2022. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi imetokana na kupungua kwa misaada ya Washirika wa Maendeleo kwa nchi nyingi za ukanda huo na kupelekea kuendelea kukabiliana na uhaba wa fedha pamoja na kuongezeka kwa gharama za ukopaji na ulipaji mdogo wa madeni; na

v. **Nchi za Afrika Mashariki** kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2022. Kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika miundombinu kupitia sekta binafsi pamoja na kuimarika kwa sekta ya utalii kwa baadhi ya nchi katika ukanda huu, zikiwemo nchi za Kenya na Tanzania zilizoonesha ukuaji mkubwa wa asilimia 5.5 na asilimia 5.2 mtawalia.

***Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Duniani***

**10.** **Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyofahamu kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma husababisha kuongezeka kwa kasi ya mfumuko wa bei hali inayoathiri nguvu ya usawa katika ununuzi ***(Purchasing Power Parity).*** Kwa ujumla kasi ya mfumuko wa bei wa dunia kwa mwaka 2023 imepungua kufikia wastani wa asilimia 6.8 kutoka wastani wa asilimia 8.7 katika mwaka 2022. Kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za chakula kumepelekea kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei. Hata hivyo, kasi ya mfumuko wa bei una sura tofauti katika maeneo mengine duniani kama ifuatavyo:

i. Kasi ya Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zilizoendelea imefikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa

asilimia 7.3 mwaka 2022 kutokana na kupungua kwa bei za vyakula na nishati;

ii. Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi, kasi ya mfumuko wa bei imepungua na kufikia wastani wa asilimia 8.3 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 9.8 mwaka 2022. Kupungua kwa mfumuko wa bei kumetokana na kupungua kwa bei za chakula na bidhaa za viwandani hasa kwa nchi ya China;

iii. Kasi ya Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara imeongezeka kufikia wastani wa asilimia 16.2 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 14.5 mwaka 2022. Hii imetokana na kupanda kwa gharama za usafirishaji wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje; na

iv. Kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kasi ya Mfumko wa Bei imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 11.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 10.4 mwaka 2022. Kutokana na kupungua kwa viwango vya mvua na ukame kwa baadhi ya maeneo ya Afrika Mashariki.

***Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar***

**11.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Nane chini ya Uongozi imara wa **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** inaendelea na juhudi za dhati za kuimarisha uchumi kwa maslahi ya wananchi kwa kuendelea kuimarisha sekta za kiuchumi na kijamii. Kwa mujibu wa viashiria vya kiuchumi, **Pato halisi la Taifa** (GDP at constant price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 3,758.8 bilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 3,499.0 bilioni mwaka 2022 sawa na kasi ya ukuaji wa asilimia 7.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2022. Aidha, Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at current price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 6,041.3 bilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 5,400.3 bilioni mwaka 2022.

**12.** **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa sababu za ukuaji wa Uchumi kwa mwaka 2023 ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa ukuaji kwa sekta ndogo ya biashara kufikia

ukuaji wa wastani wa asilimia 12.6; sekta ya fedha na bima kufikia asilimia 54.6; huduma za utawala na usaidizi kufikia asilimia 17.0; sanaa, burudani na ubunifu kufikia asilimia 33.8; usafiri na uhifadhi kufikia asilimia 9.2; sekta ya ujenzi imefikia asilimia 5.5;

ii. Kuongezeka kwa watalii waliotembelea Zanzibar kufikia watalii 638,498 mwaka 2023 kutoka watalii 548,503 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 16.4; ambao wameingiza kiasi cha TZS 59.7 bilioni ukilinganisha na TZS 51.32 bilioni kwa mwaka 2022;

iii. Kuongezeka kwa thamani ya mazao ya biashara yaliyosafirishwa nje ya nchi. Mwani wenye thamani ya TZS 19,233.2 milioni mwaka 2023 kutoka TZS 16,010.2 milioni mwaka 2022 ulisafirishwa na Karafuu zenye thamani ya TZS 47,081.1 milioni zilisafirishwa mwaka 2023; na

iv. Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji kufikia miradi 114 yenye thamani ya TZS 4,646 milioni mwaka 2023 kutoka miradi 93 yenye thamani ya TZS 4,550 milioni mwaka 2022.

**13. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2024/2025 Zanzibar inakadiriwa kufikia idadi ya watu 1,941.9 milioni ambapo kasi ya ongezeko la idadi ya watu limefikia wastani wa asilimia 3.7. Kuongezeka kwa Pato la Taifa kumepelekea kuongezeka kipato cha mtu mmoja mmoja. Wastani wa **Pato la Mtu** limefikia TZS 3.1 milioni (USD 1,241) mwaka 2023 ikilinganishwa na TZS 2.8 milioni (USD 1,235) mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 8.8.

### *Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar*

**14. Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumuko wa bei kwa mwaka 2023 imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 6.9 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2022. Kuongezeka kwa kasi ya mfumuko wa bei kumetokana na ongezeko la bei za bidhaa za chakula na zisizo za chakula katika soko. Bidhaa za chakula zimeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 6.0 mwaka 2022, na bidhaa zisizo za chakula zimefikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2022.

15. **Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumuko wa bei Zanzibar ingeweza kuwa ya juu zaidi kama Serikali isingechukua juhudi za kupunguza na kusamehe ushuru kwa baadhi ya bidhaa muhimu kama vile bidhaa ya sukari na nishati ya mafuta ili wananchi waweze kumudu kununua bidhaa hizo muhimu. Katika kipindi cha mwaka 2023/2024 Serikali ilisamehe ushuru wenye thamani ya TZS 3.89 bilioni kwa uingizaji wa bidhaa za chakula na nishati ya mafuta nchini.

**HALI YA AJIRA**

16. **Mheshimiwa Spika,** Ajira ina mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji wa ndani, hali ya utulivu pamoja na kuimarisha uchumi wa Zanzibar. Kwa mwaka 2022/2023, ajira mpya zimefikia 82,225 kutoka ajira 68,632 mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 20. Ajira kutoka Serikalini zimefikia 37,867 (wanaume ni 15,603 na wanawake ni 22,264). Ajira kutoka Mashirika ya Serikali zimefikia 6,853 (wanaume ni 4,442 na wanawake ni 2,411) mwaka 2022/2023. Kadhalika, ajira binafsi kwa 2022/2023 zimeongezeka kufikia 37,505 (wanaume ni 23,598 na wanawake ni 13,907) kutoka 24,556 (wanaume 15,947 na wanawake 8,609) kwa mwaka 2021/2022. Kuongezeka kwa ajira mpya kumetokana na uhitaji wa wafanyakazi katika sekta ya elimu (ajira mpya 22,060), ikifuatiwa na sekta ya utalii katika sekta ndogo ya Huduma za Malazi na Chakula (ajira 15,786) na Utawala wa Umma (ajira 15,501) mwaka 2022/2023.

17. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na ajira hizo, Serikali pia imeweza kuratibu ajira 3,780 nje ya nchi. Takwimu zinaoonesha kuwa vijana wa **Kizanzibari wameajiriwa kwa kazi zisizo za kitaalamu katika nchi za Qatar, Dubai na Oman. Katika mageuzi ya elimu yanayoendelea,** juhudi za makusudi zimeanza kuchukuliwa za kuwafundisha vijana fani za taaluma na ujuzi zinazohitajika ili waweze kuajiriwa katika kazi za kitaalamu na zenye tija zaidi.

## MWENENDO WA THAMANI YA SHILINGI YA TANZANIA DHIDI YA DOLA YA MAREKANI

**18.** **Mheshimiwa Spika,** Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani imepunguwa kwa wastani wa asilimia 8.2 kufikia TZS 2,506.0 kwa dola moja mwaka 2023 ikilinganishwa na TZS 2,315 kwa dola moja mwaka 2022. Hii ni kutokana na kuendelea kupanda kwa uhitaji wa dola na kupungua kwa mzunguko wa fedha za kigeni. Hata hivyo, Serikali kupitia **Benki Kuu ya Tanzania** inaendelea kuhakikisha kunakuwa na uhimilivu kwa kuendelea kuwepo kwa akiba ya fedha za kigeni ambapo hadi kufikia mwezi Disemba 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa ni zaidi ya Dola za Marekani 5.5 bilioni ambazo zinatosheleza miezi minne na nusu ya uagiziaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

## SEKTA YA UTALII

### *Uingiaji wa Watalii*

**19.** **Mheshimiwa Spika,** Utalii ni sekta kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar inayochangia asilimia 29.5 ya Pato la Taifa. Katika mwaka 2023, idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar kupitia kiwanja cha ndege na bandari imeongezeka kwa asilimia 16.4 kufikia watalii 638,489 kutoka watalii 548,503 mwaka 2022. Ongezeko hilo limesababishwa na juhudi za Serikali za kuitangaza Zanzibar kimataifa; kuongezeka kwa Mashirika mapya ya ndege yanayofanya safari za moja kwa moja Zanzibar yakiwemo Polish Airline, Azur Airline, Inter Airline, Eurowings Discover Airline, Airfrance Airline na Edelweiss Airline na kuendelea kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Nchi zilizoongoza kwa kutembelea Zanzibar kwa mwaka 2023 ni Nchi za Jumuiya ya **Ulaya** watalii 87,419 (ongezeko la asilimia 13.7); **Ufaransa** watalii 68,079 (ongezeko la wastani wa asilimia 10.7). **Italia** watalii 67,584 (ongezeko la asilimia 10.6); **Ujerumani** watalii 57,178 (ongezeko la asilimia

8.9); **Poland** watalii 46,289 (ongezeko la asilimia 7.2); **Uingereza** watalii 38,628 (ongezeko la asilimia 6) na nchi za **Afrika** watalii 38,039 (ongezeko la asilimia 5.9). Katika kuimarisha sekta hii, Serikali inafanya jitihada za kuongeza wigo wa utalii ikiwemo kuweka miundombinu kwa utalii wa mikutano, utalii wa makumbusho, utalii wa utamaduni (ikijumuisha lugha, chakula, dini, mavazi na michezo).

**SEKTA YA NJE**

21. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023, nakisi ya biashara imeongezeka hadi kufikia thamani ya TZS 1.3 trilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 1.0 trilioni mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 29. Kuongezeka kwa nakisi hii ya biashara kumetokana na uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi ambao ulifikia thamani ya TZS 1.5 trilioni mwaka 2023 ikilinganishwa na thamani ya TZS 1.2 trilioni mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 19. Miongoni mwa bidhaa zilizoagizwa nchini mwaka 2023 ni bidhaa za mashine za umeme na vifaa vyake, mashine za "nuclear reactor" na mashine za kuchemshia vifaa vya hospitali (boilers machinery) zenye thamani ya TZS 344.7 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 246.0 bilioni mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 40.

22. **Mheshimiwa Spika** Thamani ya Usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi imepungua kufikia TZS 109.2 bilioni mwaka 2023 ikilinganishwa na thamani ya TZS 180.3 bilioni mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 39 mwaka 2023. Upungufu huu umetokana na kupungua kwa usafirishaji wa zao la karafuu kutokana na msimu mdogo wa mavuno ya zao hili kufikia tani 3,197.3 zenye thamani ya TZS 47.0 bilioni mwaka 2023 kutoka tani 6,452.8 zenye thamani ya TZS 118.2 bilioni zilizosafirishwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa thamani kwa asilimia 60.2 mwaka 2023.

***Mwenendo wa Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (Intra trade)***

**23.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umeimarika kufikia thamani ya TZS 159.7 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 37.6 bilioni mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 324.2 mwaka 2023. Bidhaa zilizohaulishwa zaidi ni chuma chakavu na mafuta ya kula. Aidha, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umeongezeka kufikia thamani ya TZS 439.1 bilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 375.8 bilioni mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 17 mwaka 2023. Bidhaa zilizohaulishwa zaidi ni bidhaa za chakula ikiwemo mchele wa Mbeya, unga wa mahindi na mboga mboga.

**Ukuzaji Rasilimali**

**24.** **Mheshimiwa Spika,** Takriban miradi 114 imeidhinishwa na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa mwaka 2023, yenye thamani ya TZS 4.6 trilioni kutoka miradi 93 yenye thamani ya TZS 4.5 trilioni mwaka 2022, sawa na ongezeko la thamani kwa asilimia 2.1 mwaka 2023. Kati ya miradi hiyo, miradi 86 sawa na asilimia 75 ya miradi yote (yenye thamani ya TZS 4.4 trilioni) inamilikiwa na wageni, na miradi 28 sawa na asilimia 25 ya miradi yote (yenye thamani ya TZS 226.0 bilioni) inamilikiwa na wazawa. Aidha, upatikanaji wa miradi hii imechangia upatikanaji wa ajira mpya 6,146 kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na ajira 3,970 zilizopatikana mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 55.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 imeongezeka kufikia wanafunzi 2,502 kutoka wanafunzi 1,815 mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 37.8 Hii inatokana na kuongezeka kwa ufaulu kwa wanafunzi wenye sifa ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu. Serikali pia imeongeza fungu la mikopo kwa wanafunzi kutoka TZS 17.6 bilioni mwaka 2022/23 kufikia TZS 29.0 bilioni mwaka

2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 64.7. Vile vile, hadi kufikika Machi 2024, TZS 3.1 bilioni zilikusanywa kama marejesho ya mikopo ya elimu ya juu sawa na asilimia 84.0 ya lengo la mwaka kutoka TZS 3.0 bilioni mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 3.3.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024

**26.** **Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/2024** ulipangwa kutumia kiasi cha TZS 1,521.99 bilioni (ikijumuisha TZS 1,514.79 bilioni za miradi ya maendeleo inayotekelezwa Serikali Kuu na TZS 7.2 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa). **Programu 31** na **miradi 58 ya maendeleo** zilipangwa kutekelezwa, Programu tano (5) na Miradi tisa (9) ni ya kimkakati.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024), TZS 1,244.09 bilioni sawa na asilimia 82.1 ya fedha ilipangwa kutumika kwa kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 664.5 bilioni sawa na asilimia 62.1 ya **Bajeti ya Maendeleo** kutoka fedha za ndani na TZS 471.59 bilioni sawa na asilimia 37.9 kutoka kwa **Washirika wa Maendeleo.** Utekelezaji halisi kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024, fedha iliyopatikana ni kiasi cha TZS 1,297.91 bilioni sawa na asilimia 104.0 ya lengo la TZS 1,244.09 bilioni. Kati ya fedha hizo TZS 836.56 bilioni sawa na asilimia asilimia 108.00 ya lengo la TZS 772.5 bilioni ni kutoka Serikalini na TZS 461.52 bilioni sawa na asilimia 97.8 ya lengo la TZS 471.59 bilioni ni kutoka kwa **Washirika wa Maendeleo.**

### Utekelezaji wa Maeneo ya Kimkakati kwa Kipindi cha Miezi Tisa (Julai 2023 – Machi 2024)

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Miradi ya kimkakati ilipangwa kutekelezwa kupitia **maeneo makuu matano (5)** yaliyoainishwa katika

Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026. Miradi hiyo ilitarajiwa kuleta matokeo makubwa na kwa haraka; upatikanaji wa ajira; kuongeza uwekezaji; kuimarisha hali za wananchi pamoja na kuongeza kwa mapato ya Serikali. **Kwa Bajeti ya Mwaka 2023/2024,** kiasi cha TZS 915.87 bilioni sawa na asilimia 60.46 ya **Bajeti ya Maendeleo** ilipangwa kutumika kwa kugharamia utekelezaji wa programu na miradi ya kimkakati. Hadi kufikia Machi 2024, TZS 711.07 bilioni sawa na asilimia 104 ya bajeti iliyopangwa kwa kipindi hicho ya TZS 686.90 bilioni zilipatikana na kutumika. Kati ya fedha hizo, TZS 317.83 bilioni sawa na asilimia 91.26 ya lengo la TZS 348.25 bilioni zilipatikana kutoka Serikalini na TZS 393.24 bilioni sawa na asilimia 116 ya lengo la TZS 338.64 bilioni zilipatikana kutoka kwa **Washirika wa Maendeleo.** Utekelezaji wa programu na miradi hiyo ya kimkakati ni kama ifuatavyo:-

### A. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu

**29. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024 eneo hili lilipangiwa kiasi cha TZS 43.50 bilioni ambapo kwa kipindi cha miezi tisa, TZS 32.62 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2024, TZS 29.12 bilioni sawa na asilimia 89 ya lengo zimepatikana. Utekelezaji halisi wa miradi ya eneo hili ni kama ifuatavyo:

#### *i. Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani*

Mradi huu una lengo la kujenga bandari kubwa ya kisasa ambayo itahusisha bandari tano ikiwemo ya mizigo, eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta, bandari ya uvuvi pamoja na chelezo cha kukarabati meli. Kukamilika kwa ujenzi wa bandari hii kutasaidia kuimarika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo sekta ya uvuvi, biashara na viwanda. Hadi sasa, malipo ya fidia kwa wananchi walioathirika katika maeneo ya ujenzi na upelekaji wa miundombinu ya barabara katika mradi huu yameanza kufanyika kwa maeneo ya Kidanzini Kwa Mbara, Bumbwini yenye hekta 40 baada ya kukamilika kwa tathmini ya fidia. Vile vile, kwa wale wananchi watakaolipwa fidia kupitia nyumba 370 zinazojengwa huko Bumbwini, ujenzi wa nyumba hizo unaendelea, jumla ya nyumba 110 tayari zimejengwa

zikiwa katika hatua mbali mbali. Ujenzi huu umefikia asilimia 20 ya kazi yote. Kazi ya upelekaji wa huduma za maji na umeme zimekamilika na ujenzi wa barabara za ndani katika eneo la bandari unaendelea. Kwa upande wa eneo la Magharibi ujenzi umefikia hatua ya kuweka lami na ujenzi umefikia asilimia 35.

### *B. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu*

**30. Mheshimiwa Spika,** Eneo hili kwa mwaka 2023/2024 lilipangiwa kutekeleza miradi mitano ya maendeleo ambayo inagharimu jumla ya TZS 549.62 bilioni ambapo kwa kipindi cha miezi tisa kiasi cha TZS 812.16 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2024, TZS 479.18 sawa na asilimia 116.3 ya lengo la TZS 412.16 bilioni zimelipwa. Utekelezaji halisi wa miradi ya eneo hili ni kama ifuatavyo:

#### *i. Programu ya Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege- Pemba*

Programu hii inahusisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba kwa hatua za awali za ujenzi, ujenzi wa maegesho, njia za kupitia ndege pamoja na sehemu za kukaa abiria. Wananchi 649 kati ya 719 sawa na asilimia 90.26 tayari wamelipwa fidia katika eneo la mradi na kazi ya kufanya uhakiki wa fidia iliyobakia inaendelea ili kukamilisha ulipaji wa fidia kuwawezesha wananchi kuondoka katika eneo la mradi na kuweza kuanza utekelezaji. Kwa upande wa ujenzi, malipo ya awali ya Mkandarasi yameshafanyika.

#### *ii. Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu*

Programu inahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 407.6 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa taa na alama za barabarani Unguja na Pemba. Barabara zilizopo katika programu hii ni pamoja na Tunguu-Makunduchi km 53, Chake Chake-Mkoani km 43.5, Fumba - Kisauni km 12, Wete – Chake Chake km 22 pamoja na barabara za Kusini km 42.95. Kazi zinazoendelea kwa ujenzi wa barabara ya Wete – Chake Chake km

22 ni kuendelea na shughuli za usafishaji wa barabara iliyofanyika kwa asilimia 100; Uwekaji wa tabaka la chini la mwanzo la kifusi (G7) asilimia 80; Uwekaji wa tabaka la juu la mwanzo la kifusi (G15) asilimia 25; Uwekaji wa tabaka la pili la kifusi (G45) asilimia 32; Ujenzi wa kalvati 2; Ujenzi wa Madaraja asilimia 30 na Ujenzi wa mabomba ya kupitishia miundombinu (Service Duct) kwa urefu wa km 10. Kwa ujumla kazi ipo asilimia 25. Kwa upande wa barabara za Kusini ujenzi umefikia asilimia 92

### *iii. Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani*

Programu hii inahusisha ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Hadi Machi 2024 jumla ya km 39.15 zimeshawekwa lami kwa Unguja na 89.95 kwa upande wa Pemba km zimeshasafishwa kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kazi hizo ni sawa na utekelezaji wa asilimia 100 kwa makadirio ya kazi za kipindi hicho. Tathmini kwa ajili ya malipo ya fidia yamefanyika kwa barabara nne, uhakiki unaendelea kuweza kulipa fidia kama ulivyo utaratibu.

### *iv. Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini*

Programu hii imekusudia kujenga kilomita 100.9 za barabara za mjini kwa kiwango cha lami, njia mbili za juu (flyover), njia za wapita kwa miguu, mitaro ya maji pamoja na uwekaji wa taa za barabarani. Hadi Machi 2024, kazi ya matengenezo kwa makutano ya barabara ya Kiembe Samaki na Amani – Mtoni, barabara ya Mkapa km 8.5, uwekaji wa lami km 5.14 kwa baadhi ya maeneo umekamilika na kufanya utekelezaji kufikia asilimia 60.47. Ujenzi wa barabara ya Uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume – Kiinua Miguu – Mnazimmoja umefikia asilimia 99, kwa sasa kazi zinazoendelea ni ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji kwenye kingo za barabara pamoja na njia za kupitishia miundombinu ya mawasiliano. Barabara ya Mwanakwerekwe Gapco – Mwanakwerekwe Skuli – Kanisani Kwamchina imefikia asilimia 78. Vile vile, barabara ya Mombasa Planned Area km 6.20 ujenzi unaendelea kwa hatua ya

uwekaji wa fusi na lami; barabara ya Mpendae Planned Area km 7.35 kazi zinazoendelea ni uwekaji wa lami na utekelezaji umefikia asilimia 44.08. Aidha, ujenzi wa barabara ya Michenzani, Gongoni, Kisiwandui Msikiti Mabati – Haile Selassie ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 40. Aidha, ujenzi wa njia mbili za juu km 10.78 round about ya Mwanakwerekwe (flyover road) inaendelea kwa ujenzi wa nguzo na ujenzi wa kitako cha kuweka nguzo imefikia asilimia 25.60.

### *v. Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA)*

Mradi wenye dhamira ya kuimarisha miundombinu ya usambazaji maji safi na salama katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi "A" (Mfenesini, Masingini na Kizimbani), Magharibi "B" (Dimani na Kidutani) na Wilaya ya Kati (Jumbi- Mkorogo) pamoja na ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2024, uchimbaji wa visima 64 katika maeneo ya Dole (8), Kidutani (14), Dimani (5), Mfenesini (10), Maungani (9), Mkorogo (8) na Masingini (10), utekelezaji ni asilimia 100. Ujenzi wa matangi 15 ya maji kwa LOT 1 (Mfenesini na Dole) umefikia wastani wa asilimia 95; LOT 2 (Mkorogo, Maungani na Dimani) utekelezaji ni asilimia 98, na LOT 3 (Kidutani na Masingini) ujenzi wa matangi utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 99. Kwa upande wa ulazaji wa mabomba, kilomita 453.7 zimelazwa mabomba kati ya kilomita 466.9 sawa na asilimia 97 ya makadirio ambapo kwa LOT 1 (Mfenesini na Dole) zimefikia kilomita 176.57, na kwa LOT 2 (Mkorogo, Maungani, na Dimani) kilomita 151.34 na kwa LOT 3 (Kidutani na Masingini) kilomita 122.9 tayari zimelazwa. Majaribio ya awali yameanza kwa wananchi ambao wameshaunganishwa na huduma ya maji imeanza kupatikana katika maeneo ya Fumba, Dimani na Masingini. Ujenzi wa jengo la Ofisi Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji (MAJI HOUSE) imekamilika kwa asilimia 100 limeanza kutumika.

### vi. *Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar*

Mradi huu una lengo la kuendeleza na kuimarisha huduma ya maji safi na salama Zanzibar kwa maeneo ya Kizimbani No. 2, Jendele- Chwaka, Banda Maji, Donge, Miwani, Ndijani -Muembe Punda, Ubago - Nyakurungwi, Dunga Jumba la Mawe, Mwera-Pongwe, Chaani-Kikobweni, Mkataleni–Msufini, Mchangani-Mkiwa, Pangeni, Machui kwa Bavuai, Upenja, Kitope- Skuli na Mkokotoni. Kazi zilizofanyika ni uchimbaji wa misingi na ulazaji wa mabomba, jumla ya km 13 sawa na asilimia 50 zimelazwa mabomba ya maji kati ya kilomita 26 zilizopangwa, zabuni kwa ajili ya viungio (Pipe Fittings) imekamilika na tayari mzabuni ameshapatikana (Yumuza na Peritus.). Ujenzi wa vibanda 13 vya mashine za maji unaendelea kwa kuweka miundombinu ya umeme na maji, tarazo na dari pamoja na rangi umefikia asilimia 70. Aidha, makisio ya fedha kwa ajili ya uwekaji wa umeme mkubwa katika visima imeshawasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa malipo.

### vii. *Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)*

Mradi huu una lengo la kuimarisha sekta ya nishati kwa kujenga miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo Taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati. Katika kipindi hichi cha mapitio, kazi ya kuandaa michoro na kumtafuta mkandarasi wa ujenzi wa laini ya mkondo mkubwa wa umeme yenye uwezo wa kilovolti 132 kutoka Welezo hadi Ubago, Ubago hadi Matemwe na Ubago hadi Makunduchi pamoja na ujenzi wa kituo cha kutawanya umeme katika eneo la Welezo imefanyika. Taratibu za zabuni zinaendelea ili kumpata Mkandarasi wa umeme wa jua. Eneo kwa ajili ya uzalishaji wa umeme wa jua lenye ukubwa wa hekta 18 limeshapatikana Makunduchi. Ripoti ya tathmini imeshaandaliwa na kuwasilishwa Benki ya Dunia kwa kufanyiwa mapitio na kupata idhini (no objection) ili kuendelea na hatua nyengine za utekelezaji. Kwa upande mwengine, malipo ya fidia ya TZS 15.77 bilioni zimetolewa na Serikali kwa wananchi 1,024 watakaoathirika na utekelezaji wa mradi kwa Shehia 21.

## C. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

31. **Mheshimiwa Spika,** Eneo hili lilipangiwa kutekeleza miradi mitano kwa jumla ya TZS 272.29 bilioni kwa mwaka 2023/2024, katika kipindi cha miezi tisa kiasi cha TZS 204.22 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2024, TZS 193.81 sawa na asilimia 95 ya lengo zimepatikana. Utekelezaji halisi wa miradi ya eneo hili ni kama ifuatavyo:

### *i. Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo*

Lengo la programu hii ni kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar iwe yenye kukidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa na kuibua vipaji vya michezo Zanzibar. Kazi zilizofanyika ni ukarabati wa uwanja wa Amani pamoja na ujenzi wa viwanja vya michezo viwili vilivyo nje ya uwanja ambavyo ukarabati umefikia asilimia 95. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ukamilishaji wa milango ya maduka, hoteli na mikahawa ili kukabidhiwa kwa Serikali. Ukarabati wa Uwanja wa Gombani umefikia asilimia 97 ya utekelezaji na kazi zinazoendelea ni kufanya marekebisho katika kasoro ambazo zimejitokeza kabla ya kuukabidhi kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa matumizi. Kwa upande mwengine, viwanja vya Matumbaku Sports Complex vimekamilika na tayari vimeshafunguliwa. Maandalizi yanaendelea kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya michezo vidogo vidogo (6-in-1 multi-sports Centre) vya Wilaya za Unguja na Pemba vyenye hadhi ya Kimataifa vitakavyojengwa katika maeneo ya Mkokotoni na Tunguu eneo la SUZA kwa Unguja na Mchangamdogo na Kangani kwa Pemba. Viwanja hivyo vitajumuisha michezo ya basketball, handball, baseball, volleyball na netball. Kukamilika kwa viwanja hivyo vitaongeza vipaji vya michezo kwa vijana na kutumika kwa mashindano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kuvutia watalii wa michezo, kuitangaza Zanzibar Kimataifa na kuongeza mapato kwa Serikali.

### *ii. Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa*

Programu ina lengo la kuimarisha makaazi kwa wafanyakazi ili waweze kufanyakazi katika mazingira mazuri yenye utulivu kwa kuongeza ufanisi na kuweza kupatikana katika mazingira ya kazi wakati wa dharura. Programu hii imejumuisha Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Mkoa wa Mjini Magharibi – Lumumba; hospitali ya Wilaya ya Kaskazini "B" – Pangatupu; Wilaya ya Kati - Mwera Pongwe; Wilaya ya Kusini – Kitogani; Wilaya ya Chake Chake – Vitongoji; na Wilaya ya Wete – Kinyasini. Hadi kufikia Machi, 2024 kazi za ujenzi zinaendelea katika hatua tofauti ikiwemo usimamishaji wa nguzo na uwekaji wa matofali katika Hospitali ya Pangatupu; Mwera Pongwe - ukamilishaji wa ujenzi wa msingi "foundation"; Kitogani na Kinyasini - Wakandarasi wameanza kusimamisha nguzo kwa ajili ya kuendelea na hatua ya "superstructure". Kwa upande wa Vitongoji hatua za zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi zimekamilika na hospitali ya Mkoa – Lumumba, matayarisho ya awali ya ujenzi yameanza. Kwa ujumla ujenzi umefikia asilimia 17.4.

### *iii. Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa – Binguni*

Hospitali ya Rufaa Binguni itajengwa kupitia mkopo nafuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea. Hadi kufikia Machi 2024, hatua zilizokamilika ni pamoja na upembuzi yakinifu na utiaji wa saini baina ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Watu wa Korea tayari kwa kupata mkopo huo na kuanza ujenzi unaotarajiwa kuanza mwaka 2024/25 na kukamilika 2026/27.

### *iv. Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Elimu*

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuinua viwango na ujuzi vya wanafunzi kwa kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunza. Miradi iliyopangwa ni ujenzi wa Skuli 22 (msingi 9 na Sekondari 13)

ambao uko katika hatua mbali mbali na kufikia wastani wa asilimia 64 ya utekelezaji. Vile vile, ujenzi wa nyumba 10 za walimu kati ya nyumba 20 zilizopangwa kujengwa umeanza na kufikia asilimia 50 ya utekelezaji. Vile vile, kukamilisha ujenzi wa madarasa 12 mapya ya msingi katika maeneo ya Kisakasaka (8) na Umbuji (4) unaendelea. Ujenzi wa dakhalia katika skuli za Paje Mtule na Chwaka Tumbe umekamilika kwa asilimia 100 na ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali - Pemba unaendelea na umefikia asilimia 40. Katika programu hii, Serikali imeweza kukarabati skuli 23 za Maandalizi, Msingi na Sekondari zikiwemo Kidongo Chekundu, Chanjamjawiri, Muyuni Sekondari, Chumbuni Msingi, Faraja Sekondari, Kengeja-Dakhalia Sekondari, Kiuyu Minungwini, Chutama, Mikunguni, Fidel Castro Ukumbi, Dakhalia ya watoto wa Kiume Lumumba, Maungani, Uzini Msingi, Chaani Sekondari, Jang'ombe Maandalizi, Kizimbani Msingi, Mahonda, Ndagoni Msingi, Ole, Maziwa Ng'ombe na Mahonda, kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 35. Kwa upande mwingine ujenzi wa Majengo sita ya Ofisi za Walimu katika Wilaya ya Kaskazini A, Magharibi B, Kusini Unguja, Mkoani, Micheweni na Chake Chake kwa Pemba umefanyika sambamba na ujenzi wa Ofisi za Walimu zenye maktaba, Ofisi ya Mkaguzi wa elimu na Ofisa TEHAMA Unguja na Pemba pamoja na ununuzi wa vifaa. Kwa sasa hatua za kumtafuta Mshauri Elekezi zinaendelea kwa ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Unguja.

### *v. Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)*

Programu ina dhamira ya kuimarisha miundombinu, huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya usafi ikiwemo magari ya taka, makontena ya kuwekea taka na gari la kusafishia barabara kwa matumizi ya Mabaraza ya Miji na Manispaa Unguja na Pemba. Jumla ya loti tatu (3) kati ya 5 zinategemewa kusambaziwa vifaa hivyo na loti mbili (2) zilizobaki zitapatiwa vifaa baada ya kukamilika kwa hatua za zabuni ambazo zitawezesha kupata Mzabuni atakaefikia vigezo vilivyowekwa. Vile vile, makubaliano

na Mzabuni aliyeshinda katika kazi ya upembuzi yakinifu wa uendelezaji wa urithi wa kihistoria Mji Mkongwe (Green Corridor) yamefikiwa. Kwa sasa kazi ya kufanya tathmini ya zabuni ya mradi wa kuyaendeleza Maeneo yanayokuwa kwa kasi Zanzibar inaendelea. Ujenzi unategemea kuanza Aprili 2024. Kampuni ya kujitegemea (Independent RAP Monitor) imepatikana kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia malipo ya fidia. Kamati za kushughulikia malalamiko wakati wa ulipaji wa Fidia na wakati wa utekelezaji wa Mradi wa AUP-Unguja zimeandaliwa pamoja na kutoa mafunzo ya njia za kurikodi na kuwasilisha malalamiko kwa Kamati zinazoshughulikia malalamiko hayo ikiwa ni sharti la msingi kwa miradi inayopata mkopo au ruzuku kutoka Benki ya Dunia.

### *D. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimili*

32. **Mheshimiwa Spika,** Eneo hili lilipangiwa kutekeleza miradi mitatu kwa jumla ya TZS 75.08 bilioni, kwa kipindi cha miezi tisa kiasi cha TZS 56.31 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2024, kiasi cha TZS 20.28 bilioni sawa na asilimia 36.0 ya TZS 56.31 bilioni zimelipwa. Utekelezaji halisi wa miradi ya eneo hili ni kama ifuatavyo:

#### *i. Mradi wa kuimarisha Ulinzi na Usalama*

Mradi una lengo la kuimarisha ulinzi na usalama kwa kufikia viwango vya Kimataifa ili kuweka mazingira salama kwa wananchi na wageni katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Kazi zilizoanza ununuzi na usambazaji wa vifaa vya usalama kutoka kwa Wazabuni walioshinda kwa mujibu wa Mkataba ulioidhinishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mradi huu utasaidia kuimarisha ulinzi, utawala na kuongeza mapato ya Serikali kutokana na kuongezeka kwa Watalii, kuongeza ajira na kipato kwa wananchi.

### *ii. Ujenzi wa Mji wa Serikali Zanzibar*

Mradi wa ujenzi wa Mji wa Serikali una lengo la kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi ili waweze kutoa huduma bora na zenye ufanisi. Mradi umepanga kujenga Ofisi mpya za Serikali katika eneo la Kisakasaka. Kazi zilizofanyika ni kutayarisha michoro pamoja na usafishaji wa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**33. Mheshimiwa Spika,** Maelezo ya kina ya Utekelezaji kwa programu na mradi ya maendeleo ikiwemo ya kimkakati iliyotekelezwa kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024 yanaonekana katika Kitabu cha Kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi 2023 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/24 kilichosambazwa kwa wajumbe wote kwa njia ya nakala laini na ngumu.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024 NA MPANGO WA MAENDELEO WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2024/2025

### Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

**34. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024 Ukuaji wa uchumi wa Dunia unatarajiwa kuendelea kuimarika kufikia kasi ya ukuaji wa wastani wa asilimia 3.2 sawa na ukuaji wa mwaka 2023. Hii ni kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi wa Aprili 2024.

### Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar

**35. Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar mwaka 2024 unatarajiwa kuimarika kutokana na hatua za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 ambayo kwa ujumla inatekeleza Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050. Sekta za kiuchumi na kijamii zinazotarajiwa kuendelea kuimarika zaidi ni pamoja na sekta ya elimu, miundombinu, afya na ustawi wa jamii, kilimo, uvuvi, utalii, biashara na viwanda.

## MALENGO NA SHABAHA ZA UCHUMI JUMUISHI KWA MWAKA 2024

36. **Mheshimiwa Spika,** Shabaha za Uchumi Jumuishi zilizozingatiwa katika Mpango wa mwaka 2024 ni kama ifuatavyo: -
    i. Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.2 mwaka 2024;
    ii. Mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya kiwango cha asilimia 5 kama ilivyo shabaha iliyowekwa kwa nchi za Afrika Mashariki;
    iii. Uwiano wa Mapato ya ndani kufikia asilimia 39.1 ya Pato la Taifa mwaka 2024 kutoka asilimia 26 mwaka 2023;
    iv. Uwiano wa Mapato ya kodi kufikia asilimia 33 ya Pato la Taifa mwaka 2024 kutoka asilimia 22.4 mwaka 2023;
    v. Uwiano wa Deni na Pato la Taifa kufikia asilimia 15 mwaka 2024 kutoka asilimia 13 mwaka 2023;
    vi. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2024 ili kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
    vii. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024, Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.2 kutoka ukuaji wa asilimia 7.4 mwaka 2023 matarajio ya ukuaji huo utatokana na sababu zifuatazo:-
    i. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa asilimia 30 kutoka watalii 638,498 kwa mwaka 2023 hadi watalii 829,929 kwa mwaka 2024 kwa wageni wa Kimataifa (international tourists) na kuongezeka kwa watalii wa ndani kwa asilimia 64.5 kutoka watalii 164,084 mwaka 2023 hadi kufikia watalii 270,000;
    ii. Kuendelea kutekelezwa kwa Miradi mikubwa ya Kimkakati ya maendeleo na miradi mengine itakayochangia ukuaji wa uchumi ikiwemo miundombinu ya barabara, afya, elimu, viwanja vya michezo, maji safi na salama;
    iii. Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili ubaki katika tarakimu moja;

iv. Kuongezeka kwa uhamasishaji wa ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa matumizi ya Serikali;
v. Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza thamani na miradi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;
vi. Kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta za uchumi wa Buluu kama vile kuimarisha Matumizi Endelevu ya Bahari;
vii. Kuwawezesha Wajasiriamali kwa kuwapatia elimu, uelewa na ufahamu zaidi, ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana za ujasiriamali, uongezaji wa thamani wa mazao ya baharini, upatikanaji wa mitaji, masoko pamoja na kuchangia katika sekta ya uvuvi, mazao ya baharini ikiwemo mwani;
viii. Kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi kutokana na juhudi za Serikali za kukuza uwekezaji, uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira.

**38. Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya ukuaji huo unategemea na misingi ifuatayo:

i. Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha;
ii. Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo;
iii. Kuendelea kuimarika kwa miundombinu na huduma za bandari zetu ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu; na
iv. Kuendelea kuwepo kwa hali ya usalama nchini, nchi jirani na nchi nyengine duniani.

**39. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuweka utulivu wa bei kwa wananchi ikiwemo:-

i. Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;
ii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kutunza thamani ya Shilingi ya Tanzania na kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei;
iii. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Serikali itaendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine Duniani;

iv. Kuendelea kushajihisha na kuimarisha shughuli za uzalishaji viwandani;

v. Kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini; na

vi. Kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku hasa kwa vyakula vikuu vinavyolimwa hapa nchini.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/2025

**40. Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/2025, ni mwendelezo wa utekelezaji wa malengo ya Serikali yaliyowekwa katika Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025 na Maelekezo na Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anazozitoa katika Hotuba zake anapokutana na wananchi. Mpango huu unatarajiwa kutekeleza miradi na programu zenye azma ya kufikia malengo hayo na kutoa matokeo chanya katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya kuifanya kuwa Nchi ya Kipato cha Kati cha Juu ifikapo mwaka 2050 (*Upper Middle-Income Status*).

### Maeneo ya Kimkakati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**41. Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2024/2025, miradi ya kimkakati imepangwa kwa kuzingatia umuhimu na faida zitakazopatikana na imegawanywa katika maeneo matano (5) kama ulivyo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Miaka Mitano 2021– 2026 ambayo ni: (1) Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu; (2) Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu; (3) Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi; (4) Kukuza Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; na (5) Kuimarisha Utawala na Uhimili. Utekelezaji wa miradi hii unatarajiwa kugharimu kiasi cha TZS 2,087.71 bilioni sawa na asilimia 63.98 ya bajeti ya maendeleo ya TZS 3,263.07 bilioni.

### I. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu

42. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya uchumi wa buluu katika ukuaji wa Taifa na maslahi ya wananchi kiujumla, Serikali itaendelea kutilia mkazo katika utekelezaji wa sera na mikakati ya kuendeleza Utalii wa Baharini na Visiwani kwa kushajihisha Miradi ya Uwekezaji katika Visiwa, kuendeleza Ujenzi wa Hoteli za Nyota Tano, kuweka miundombinu ya kufanikisha michezo ya bahari pamoja na kuanza maandilizi ya usafiri wa baharini (sea taxis). Pia itaimarisha Uvuvi na Rasilimali za Bahari kwa Kuimarisha mazingira ya bahari, kusimamia upatikanaji wa meli za uvuvi, kujenga uwezo wa usimamizi wa rasilimali za bahari, kuimarishwa kwa upatikanaji wa mazao ya baharini ikiwemo ukulima wa mwani, kusimamia upatikanaji wa mifumo ya kuhifadhia mazao ya baharini sambamba na kuendelea na ujenzi wa madiko na masoko ya samaki ya kisasa.

43. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, katika eneo hili miundombinu ya Bandari itaendelezwa ambapo Serikali imedhamiria kuanza ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani, kusimamia na kuratibu ujenzi wa jengo la abiria la Mpigaduri na bandari ya mizigo ya Fumba. Kwa umuhimu wa kipekee Serikali itaendelea kuiimarisha Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa kuimarisha Kampuni ya Mafuta ya Zanzibar (ZPDC) pamoja na kusimamia uwekezaji wa miundombinu ya uhifadhi wa mafuta na gesi huko Mangapwani. Takriban TZS 453.03 bilioni zinatarajiwa kutumika kutekeleza shughuli hizo.

### II. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu

44. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na kasi yake ya kuimarisha miundombinu ya usafiri wa anga, nchi kavu na majini. Kwa mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea na Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Pemba, Ujenzi wa jengo la **Abiria Terminal II A.A.K.I.A,** ujenzi wa barabara mbali mbali Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 782.9 zikiwemo barabara kuu, mijini, vijijini na za ndani, ujenzi wa vituo vya mabasi na ujenzi wa kituo na maegesho ya vyombo vya usafiri katika soko la Mwanakwerekwe.

45. **Mheshimiwa Spika** Katika kuhakikisha Taifa linakuwa na upatikanaji wa huduma za umeme na maji kwa uhakika na salama, Serikali itahakikisha ukamilishaji wa miundombinu ya maji pamoja na usambazaji, kuimarisha upatikanaji wa miundombinu na huduma za umeme ikiwemo upatikanaji wa umeme mbadala.

Vile vile, miundombinu mbali mbali ya utalii itaimarishwa ikiwemo maeneo ya kihistoria, ili kuweza kuwavutia watalii zaidi sambamba na kuimarishwa kwa miundombinu ya Mji Mkongwe ambao ni kivutio kikubwa cha watalii hapa nchini. Takriban TZS 811.10 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kutekeleza shughuli hizo.

### III. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi

46. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Taifa linakuwa na uchumi wa kidigitali miundombinu ya uchumi wa kidigitali itaendelea kuimarishwa sambamba na uimarishwaji wa mifumo ya usimamizi wa fedha na uendeshaji wa shughuli za Serikali. Serikali itaendelea kuimarisha biashara na viwanda kwa kuweka miundombinu kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya viwanda na kuyaimarisha maeneo huru ya kiuchumi ili kuweza kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Takribani TZS 65.32 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kutekeleza shughuli hizo.

### IV. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

47. **Mheshimiwa Spika,** Upatikanaji wa huduma bora na sahihi za kijamii ni miongoni mwa viashiria muhimu katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa. Kwa mwaka 2024/2025, kwa upande wa sekta ya afya Serikali itaendelea na uimarishaji wa miundombinu ya afya kwa kuendelea na Ukarabati na utanuzi wa Hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja, Ujenzi wa nyumba za madaktari, Ujenzi wa Hospitali ya Binguni, Ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya. Kwa upande wa sekta ya elimu Serikali itaendelea kutekeleza Mageuzi ya Sekta ya Elimu kwa Ujenzi wa dakhalia za wanafunzi, Ujenzi wa Madarasa 1,000, Ukarabati wa skuli na **Utanuzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).**

**48. Mheshimiwa Spika** Sekta ya Makaazi itaimarishwa kwa kuendelea na Ujenzi wa nyumba za bei nafuu katika maeneo ya Kwamchina, Chumbuni, Mfikiwa na Finya na kuendeleza Sekta ya Habari na Michezo kwa kuendelea na miundombinu ya Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya na Ujenzi wa Jengo la ZBC na Tume ya Utangazaji. Takribani TZS 674.62 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kutekeleza shughuli hizo.

## V. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimili

**49. Mheshimiwa Spika,** Mafanikio ya kiuchumi na kijamii hayawezi kufikiwa pasipo na Amani na usalama. Bila ya Amani hakuna maendeleo. Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kuhakikisha nchi inaendelea kubakia katika hali ya utulivu na amani zaidi. Katika eneo hili Serikali imekusudia kuweka mazingira mazuri ya kutoa na kupokea huduma kwa kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Serikali, kuanza ujenzi wa Mji wa Serikali, pamoja na Ujenzi wa ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Ofisi za Masheha. Aidha, Jitihada za kuimarisha utawala bora kupitia upatikanaji wa haki za raia na usawa zinaendelea kupewa kipaumbele ambapo Serikali kwa sasa inaendelea na Ujenzi na Ukarabati wa Mahkama za Wilaya na Mikoa Unguja na Pemba sambamba na uwekaji wa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa kesi. Takribani TZS 83.62 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

**50. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali inatarajia kutekeleza Miradi mengineyo ambayo itagharimu TZS 1,175.35 bilioni. Miradi mengineyo ni Miradi inayoendelea, malipo ya fidia na upelekaji wa miundombinu katika maeneo yanayotarajiwa kutekelezwa miradi ya kimkakati.

## RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/2025

**51.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025, Serikali imepanga kutumia kiasi cha TZS 3,271.11 bilioni (TZS 3,263.07 kwa miradi ya Serikali Kuu na TZS 8.03 bilioni kwa miradi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa) sawa na asilimia 63.11 ya bajeti yote ya Serikali kwa kutekeleza shughuli za maendeleo. Mpango wa Maendeleo wa Serikali Kuu unategemewa kugharimu TZS 3,263.07 bilioni ambapo TZS 1,862.0 bilioni sawa na asilimia 57.06 ya bajeti yote ya maendeleo ni kutoka Serikalini na TZS 1,401.07 bilioni (TZS 1,093.31 bilioni ni mikopo na TZS 307.76 bilioni ni ruzuku) sawa na asilimia 42.94 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Fedha hizi zitatumika kugharamia utekelezaji wa programu 34 na miradi 63 kama ilivyoainishwa katika katika kitabu cha pili (*Mwelekeo wa Hali ya uchumi wa Zanzibar 2024 na Mpango wa Maendeleo wa 2024/2025*). Aidha, miradi mingine ya maendeleo, itaendelea kugharamiwa na sekta binafsi na utaratibu wa Mashirikiano (Ubia) kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

## MAENEO MTAMBUKA

### Uandaaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050

**52.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Jamhuri ya Muungano inatarajia kukamilisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025. Hivyo, kupitia Wizara ya Mipango na Uwekezaji ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Tume ya Mipango Zanzibar inaendelea na uratibu wa maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050). Hatua za maandalizi ya Dira 2050 zilizinduliwa rasmi tarehe 03 Aprili, 2023 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Kufuatia kuteuliwa kwa timu ya Wataalamu iliyotangazwa mwezi Disemba, 2023 ili kuandika Dira hiyo, kwa sasa Wizara kupitia Tume ya Mipango iko katika zoezi la kupata maoni ya wadau ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050.

**Masuala ya Idadi ya Watu**

53. **Mheshimiwa Spika,** Utambuzi wa idadi ya watu katika eneo husika au nchi ni jambo muhimu sana katika kupanga mipango ya maendeleo. Matokeo ya Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2022, yanaonesha kuwa Zanzibar ina jumla ya watu 1,889,773 na kasi ya ukuaji wa Idadi ya watu ni asilimia 3.7. Mkoa wa Mjini Magharibi ulibainika kuwa na idadi kubwa ya watu wapatao 893,169 ambayo ni asilimia 47.3 ya watu wote wa Zanzibar. Katika kuzingatia matumizi sahihi ya matokeo ya Sensa Tume ya Mipango imeanzisha utaratibu wa kuwajengea uwezo maofisa mipango wa taasisi tofauti juu ya kuoanisha viashiria vya masuala ya idadi ya watu katika mipango na bajeti. Aidha, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Tume ya Mipango imeweza kutoa uhamasishaji wa matumizi ya takwimu za sensa kwa makundi mbalimbali Unguja na Pemba na umuhimu wa kutumia takwimu za idadi ya watu ili kuweza kufanya maamuzi sahihi juu ya mipango ya maendeleo kwa kuangalia idadi ya watu iliopo, rasilimali zinazohitajika na mipango ya baadae. Vile vile, katika mwaka 2023/2024, Tume ya Mipango imeandaa rasimu ya Sera ya Idadi ya Watu na Maendeleo ambayo itatoa muongozo kamili juu ya usimamizi wa masuala ya idadi ya watu Zanzibar.

54. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2024/2025 itaendelea na kutoa matokeo maalumu ya Sensa kwa kutoa ripoti za uchambuzi kwa hali halisi ya vizazi na vifo, hali ya Elimu, hali ya ulemavu, uhamiaji na nguvu kazi ya uhamaji na hali ya kijamii na kiuchumi kwa kila Mkoa.

**Tafiti na Ubunifu kwa Maendeleo**

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa tafiti kwa maendeleo, Serikali imeanza kutumia matokeo ya tafiti na ubunifu kuimarisha sera na kutoa majibu ya kisayansi. Mfumo wa kuhifadhi taarifa za tafiti na ubunifu umetengenezwa, kiasi cha tafiti 350 zimehifadhiwa katika mfumo. Hatua zinazoendelea ni kuwapatia

mafunzo watafiti ili waweze kufanya tafiti za kimkakati kwa mujibu wa vipaumbele vya tafiti kitaifa (**Zanzibar Research Agenda 2020-2025**) pia waweze kupata fedha kwa wafadhili wanaofadhili utayarishaji wa tafiti katika maeneo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) Zanzibar imefungua kituo mama cha Ubunifu Maruhubi kinachoitwa iBUA Innovation Hub kusaidia wabunifu hasa vijana waweze kujiajiri wenyewe na kukuza vipaji vyao. Tafiti na ubunifu zitaweza kuleta mbinu mpya za uzalishaji na kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi. Tunaziomba Wizara/Idara na Taasisi za Serikali na binafsi kulipokea na kulipa msisitizo suala la tafiti na ubunifu ili Serikali iweze kutatua changamoto za maendeleo kwa ushahidi wa tafiti.

**Uhifadhi wa Mazingira.**

**56.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Mei 2024, Serikali imeweza kutekeleza miradi mikuu minne ikiwemo kujenga tuta lenye urefu wa mita 450 la kuzuia maji ya bahari kuingia katika maeneo ya Kilimo katika eneo la Tovuni, Pemba kupitia Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za Pwani ya Zanzibar. Mradi wa kuwapatia mbinu mbadala za kujikimu kimaisha wananchi walioko katika maeneo yalioathirika na mabadiliko ya tabianchi hususan katika sekta ya Kilimo. Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Mfumo wa Ikolojia umeweza kununua boti sita na vifaa vyake vya uvuvi na kukabidhiwa kwa Kamati za uvuvi katika Shehia ya Mbuyu Tende, Kijini na Jugakuu.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali katika mwaka wa fedha 2024/25 imepanga Kutayarisha Mpango wa Kitaifa wa Mazingira (Environmental Master Plan); Kuongeza uelewa kwa jamii juu ya uhifadhi wa Mazingira kupitia Mikutano, Vipindi vya Redio na Televisheni; Kutayarisha Kanuni/Miongozo ya Kimazingira. Vile vile kutambua na kujua hali halisi ya mabwawa na michirizi ya maji katika maeneo mbali mbali ya Pemba.

**Makundi yenye Mahitaji Maalum**

**58.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu imefanikiwa kupata msaada wa vifaa saidizi kutoka katika Kampuni ya Cigarette Tawi la Zanzibar waliopo Mbweni ikiwemo Baskeli nne za maringi matatu (Triycle), Magongo ya mkononi 40, Magongo ya kwapani 40, Fimbo nyeupe 28 pamoja na Mashine za charahani 30. Kadhalika, Baskeli za maringi mawili na Wheelchair 10 zimepokelewa kutoka katika Kampuni ya Al-ataa ya nchini Kenya. Vile vile visaidizi 30 vya Watu wenye Ulemavu vikiwemo viti vya magurudumu mawili 12, baskeli ya magurudumu matatu 10, fimbo za kutembelea 5 na miwani 3 vimepokelewa kutoka kwa Al-Wadoud Charitable Group. Katika kipindi hiki cha mwaka 2024/25, Serikali kupitia Baraza la Taifa la watu wenye ulemavu itahakiksha inajenga uwelewa wa Sheria Namba 8/2022 ili kupata miongozo ambayo itasaidia katika kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Baraza la Taifa la watu wenye ulemavu litahakikisha linaimarisha mashirikiano kwa taasisi za ndani na nje na wadau wa maendeleo ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za msingi. Baraza linaendelea na kunyanyua uchumi wa Watu wenye Ulemavu kwa kuwapatia misaada na mitaji ya kuanza biashara, kuwalipia ada za masomo na kuwapatia msaada wa vifaa saidizi kutoka katika Kampuni na Taasisi tafauti ili kuhakikisha tunakuza haki na fursa kwa watu wenye ulemavu.

**59.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Tume ya Ukimwi inaendelea kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI kwa kutumia mikakati na programu tafauti, katika jitihada hizo Serikali imeweza kupunguza maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI kutoka watu 499 waliopata maambukizi mapya mwaka 2012 hadi watu 117 kwa mwaka 2023. Vile vile, vifo vinavyotokana na maradhi ya UKIMWI vimeweza kupungua kutoka vifo 682 mwaka 2012 hadi vifo 107 mwaka 2023. Aidha, Serikali imefanikiwa kudhibiti kiwango cha watu wanaoishi na VVU kwa kuendelea kubaki kuwa chini ya asilimia 1 kama ilivyobainishwa katika utafiti wa mwaka 2023 ambapo ni asilimia 0.4 ya watu ambao wanaishi na Virusi vya

UKIMWI. Katika kipindi kijacho, Tume ya Ukimwi itafanya mapitio ya Sera na Sheria ya UKIMWI ili iendane na uhalisia wa mazingira ya sasa. Pia, kuisambaza Miongozo iliyoandaliwa ya Uzingatiaji wa Masuala ya UKIMWI sehemu za kazi kwa wadau wote na kuwepo kwa Mpango maalum wa upatikanaji wa rasilimali fedha endelevu.

**Mipango ya Kuendeleza Watenda Kazi**

60. **Mheshimiwa Spika,** Taaluma na ujuzi ni vitu muhimu ambavyo watu wamewekeza katika maisha yao na kuwezesha kuwa miongoni mwa wazalishaji wabobezi katika jamii. Serikali inaendelea kuimarisha rasilimali watu ili kuleta tija na manufaa katika jamii. Katika kufanikisha hilo, Tume ya Mipango inakusudia kufanya utafiti wa hali ya utumishi Zanzibar ili kuweza kubaini changamoto na mahitaji ya wataalamu wanaohitajika kwa sasa na baadae. Sambamba na hayo jitihada za kutoa uelewa zinaendelea kwa kuwaandaa watenda kazi wa baadae kufanya maamuzi sahihi wakiwa katika ngazi za elimu ya sekondari ili waweze kuzitambua kada adimu na fani za vipaumbele kwa mujibu wa mahitaji ya soko la ajira linalotokana na Dira na Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Vile vile, Zanzibar katika kufikia azma ya Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar (ZADEP) 2021- 2026 Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Tony Blair imeanza mpango wa kuwajengea uwezo watendaji wa Taasisi za Serikali juu ya masuala ya umuhimu wa kutumia Mfumo wa taarifa za kijiografia (Geographical Information) ambao utaonesha matokeo kwa picha za Satellite kwa ajili ya kupanga, kufanya bajeti na kutoa maamuzi sahihi yenye ushahidi.

**UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI**

61. **Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo ni moja ya nyenzo muhimu inayopima ufanisi wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo kwa kubainisha mafanikio na changamoto. Tume ya Mipango itaendelea kutumia mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini kwa

kutumia viashiria vilivyoainishwa katika Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP M&E Framework) 2021–2026 ili kupima utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 na kuchukua hatua stahiki za kufikia malengo ya utekelezaji kwa muda uliopangwa. Miongozo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango ikiwemo Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 na Sheria ya Fedha ya mwaka 2016, itaendelea kuzingatiwa. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E System) utaimarishwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za ufuatiliaji na tathmini ili kupata matokeo tarajiwa.

62. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza malengo na mikakati ya Maendeleo Kikanda na Kimataifa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kumi na saba (17). Kwa mwaka 2023/24 Zanzibar iliwasilisha Ripoti ya utekelezaji wa malengo ya SDGs Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ripoti iliyowasilishwa Umoja wa Mataifa, malengo yaliyopewa mkazo zaidi ni Malengo matano (5): **Lengo nambari 1**, Kuondoa umaskini katika aina zake zote kila mahali; **Lengo nambari 2,** Kukomesha njaa, kufikia usalama wa chakula na kuboresha lishe na kukuza kilimo endelevu; **Lengo nambari 13**, Kuchukua hatua za haraka kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na athari zake; **Lengo nambari 16**, Kukuza jamii zenye amani na umoja kwa maendeleo endelevu, kutoa upatikanaji wa haki kwa wote na kujenga taasisi zenye ufanisi, uwajibikaji na umoja katika ngazi zote na **Lengo namba 17**, Kukuza Ushirikiano wa Kimataifa kwa Maendeleo Endelevu. Kwa upande wa utekelezaji wa Ajenda za Afrika 2063 (African Agenda 2063) utekelezaji wake unakwenda sambamba na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mafanikio katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Ajenda za Afrika yanaonekana katika Programu na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Serikali ambayo imeanza kuleta tija kwa wananchi.

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa kufanikisha Ufuatiliaji na Tathmini kwa Programu na Miradi ya Maendeleo, Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar unaendelea kutumika kwa ajili ya kuongoza wadau wote wa maendeleo kutekeleza maeneo ya Kimkakati na Kipaumbele kwa kupima Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Muongozo huu ni wa miaka mitano 2021–2026 ambao una lengo la kupima matokeo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa ajili ya kufikia Malengo na Mikakati iliyoundwa.

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa Ufuatiliaji na Tathmini, Tume ya Mipango imeandaa rasimu ya Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya kutoa muongozo na kusimamia maswala yote yanayohusu Ufuatiliaji na Tathmini nchini. Sera hiyo ipo katika ngazi za kimaamuzi kwa kupata ridhaa kwa ajili ya kuanza kutumika. Aidha, mafunzo ya uelewa wa Sera hiyo yatatolewa kwa Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na sekta binafsi ili kila Sekta ifahamu na kuweza kuitumia kwa maendeleo ya dhana ya Ufuatiliaji na Tathmini nchini kwa ajili ya kuleta uwajibikaji katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo.

65. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kufanya mapitio ya Mpango wa Kati wa Maendeleo (ZADEP) 2021-2026 kwa kufikia nusu ya kipindi cha utekelezaji wake (miaka mitatu) ili kufanya uchambuzi kuweza kujua mafanikio, changamoto na kuja na mapendekezo ya kuishauri Serikali. Kazi ya uandaaji wa Rasimu ya Ripoti ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kufikia mwaka 2023 inaendelea na inatarajiwa kuwasilishwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuunganishwa na ya Tanzania Bara na kupata Ripoti moja ya Kitaifa kwa kuwasilishwa Umoja wa Mataifa.

66. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uwezo wa maafisa Ufuatiliaji na Tathmini katika Taasisi zote za Serikali, Tume ya Mipango inaendelea na kutafuta ufadhili kwa Washirika wa

Maendeleo kwa lengo la kuzijengea uwezo Taasisi kiutendaji ili kutumia miongozo ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kuripoti Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo. Aidha, Tume ya Mipango Zanzibar, inaendelea kuwakaribisha watendaji kutoka Taasisi za Serikali na Binafsi wanaotaka kujengewa uwezo katika shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini kufika katika Ofisi za Tume kama inavyofanywa na baadhi ya Taasisi kuleta watendaji wao ili kujengewa uwezo.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** katika kufanikisha shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini katika utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo, Tume ya Mipango Zanzibar inaratibu Kongamano la Kitaifa la Wiki ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza (MEL WEEK) litakalofanyika Septemba 2024 hapa Zanzibar. Kongamano hili la siku tano (5) ambalo hufanyika kila mwaka Tanzania lina lengo la kuendeleza juhudi za Serikali za Kujenga Uelewa na Utamaduni wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa Watendaji wa Serikali, Taasisi Binafsi, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendelo na Jamii kwa ujumla. Vile vile, kongamano hilo linaunga mkono juhudi za viongozi wetu wa Kitaifa katika kuendeleza na kuhamasisha shughuli za Utalii na kukuza uchumi nchini.

## MAJUMUISHO

**68.** **Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inayoelezea Mpango wa Maendeleo wa Taifa ndiyo msingi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 ambayo Serikali itaiwasilisha baadae leo katika Baraza hili Tukufu. Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Mwaka 2024/2025 umezingatia dhana ya ushirikishwaji wa wadau katika hatua za uandaaji wa Mpango wa Maendeleo na maamuzi katika ngazi zote Serikalini. Ni vigumu kuwataja wadau wote waliotoa maoni na ushauri hadi kufikia hapa lakini mchango na maoni yao tumeyazingatia na ni sehemu ya Mpango huu wa Maendeleo. Kwa kutambua mchango na umuhimu wa sekta binafsi, Mpango huu umeipa sekta binafsi umuhimu wa kipekee. Vile vile, Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili

kuongeza miradi ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) katika kugharamia utekelezaji wa mpango.

69. **Mheshimiwa Spika,** Utulivu na amani katika nchi ni kitu muhimu sana na chenye thamani ya kipekee na inahitaji kulindwa kwa nguvu zetu zote. Kwa hili na kwa nafasi ya kipekee, nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa juhudi zake kubwa za kuhakikisha kuwa nchi yetu inabakia katika hali ya amani na utulivu kwa maslahi ya wananchi wote. Kupitia fursa hii naomba pia kuwashukuru wajumbe wote wa Tume ya Mipango, Kamati ya Wataalamu na Sekretariati yake kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kushauri, kutoa miongozo na maelekezo yao katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Mipango Mikuu ya Maendeleo ya Kitaifa ikiwemo ya kiuchumi, uwekezaji na masuala ya kijamii. Maoni na maelekezo yao ndio msingi wa kuibua maeneo mapya ya kuyafanyia kazi kwa maslahi ya nchi yetu katika kuimarisha uchumi na kupunguza umasikini kwa wananchi wote.

70. **Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa nisisitize suala zima la Uzalendo. Ni jambo muhimu kwa wananchi kuwa nalo na kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni na kutekeleza miradi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu sambamba na uwajibikaji ndani ya utumishi wa umma. Naomba pia, nitoe wito kwa kila sekta kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa zinatekelezwa ipasavyo katika eneo lake la kiutendaji. Vile vile, wito kwa wananchi kufanya juhudi ya kutekeleza kwa vitendo malengo ya Dira na kuhakikisha yanafikiwa katika kiwango cha kilichokusudiwa ifikapo mwaka 2050. Aidha, niwaombe wananchi wote wa Zanzibar kushiriki kikamilifu katika uandaaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 Tanzania ikiwemo kutoa maoni yao juu ya mwelekeo wa Taifa tunalolitarajia.

**HITIMISHO**

71. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati na kwa niaba ya Serikali ninaomba kutumia fursa hii adhimu ya kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge, Madiwani, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Washirika wa Maendeleo na Wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika mipango, utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na kujenga uchumi wa nchi yetu. Ushiriki wao wa dhati umewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ninawaomba waendelee kutupa ushirikiano katika kutekeleza Mpango huu ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Pia, nawashukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Idara zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao.

72. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nitoe shukrani za dhati kwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango Mheshimiwa Juma Makungu Juma ambaye ni msaidizi wangu wa karibu kwa umakini wake, busara na weledi katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu. Ninawashukuru pia, Makamishna wa Tume ya Mipango na watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dkt. Rahma Salim Mahfoudh. Vile vile, niwashukuru Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango Dkt. Juma Malik Akil, Naibu Katibu Mkuu Nd. Aboud Hassan Mwinyi na Mhasibu Mkuu wa Serikali Nd. Hamad Saleh Hamad kwa kufanyakazi kwa karibu na Tume ya Mipango. Aidha, natoa shukurani za dhati kwa Makatibu Wakuu wa Wizara za SMZ wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi Mhandisi Zena Ahmed Said kwa ushirikiano wanaotupatia katika kufanikisha majukumu yetu. Ni matumaini yangu kwamba tutaendelea kushirikiana katika kutekeleza mipango yetu na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa kazi za kila siku.

73. **Mheshimiwa Spika,** kwa aina ya kipekee naomba niwatambue na kuwashukuru Washirika wa Maendeleo wa Kitaifa, Kimataifa na

Nchi Wahisani kwa misaada ya kifedha na kiutaalamu wanaoendelea kutupatia. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo wa ndani kama ifuatavyo: PBZ, ZSSF, ZANZIBAR MILELE FOUNDATION, NMB, NBC, CRDB na COSTECH. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo wa nje na nchi rafiki zinazoendelea kushirikiana nasi ni pamoja na ACRA, AF, AFD-FRANCE, AfDB, AMREF, AUSTRIA, BADEA, BELGIUM, CHINA, CANADA (CIDA), DANIDA, DfID, EDF, EU, EXIM BANKS za India, China na Korea, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, GERMANY (GIZ AND KfW), GPE, GOOD NEIGHBOURHOOD, HIPZ, IAEA, INDIA, IFAD, ILO, IMF, IRELAND, JAPAN (JICA), KHALIFA FUND, MFUKO WA MAENDELEO WA UMOJA WA FALME ZA KIARABU (UAE), KOREA, KUWAIT, MALAYSIA, NORWAY, OMAN, OPEC FUND, PMI, QATAR CHARITY ORGANISATION, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, STBF, SWEDEN, THPS, TfT, UK, UKEF/CITI BANK NA DEUTCH BANK, UN, UNDP, UNEP, UNFPA, UNESCO, UNICEF, UNIDO, USAID, UN WOMEN, UTURUKI, WORLD BANK na WHO. Kipekee naomba nitoe shukrani kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kushirikiana na Zanzibar katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

74. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kumaliza hotuba yangu hii, napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wawakilishi na Wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inaambatanishwa na vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2023 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/2024 na Mwelekeo wa Hali ya uchumi wa Zanzibar 2024 na Mpango wa Maendeleo wa 2024/2025 ambavyo vina taarifa na uchambuzi wa kina pia vinapatikana katika tovuti ya Tume ya Mipango (http. planningznz.go.tz)

75. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa Baraza lako Tukufu lipokee na kujadili Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2024/2025.

**76. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima naomba kutoa hoja.

**DKT. SAADA MKUYA SALUM**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS – FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR.**